KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 22, Issue 3

27th Jumaadal Aakhira 1433

18th MAY, 2012

ANAESTAHIKI KUTEREMSHA MWILI WA MAITI KABURINI

NA: SHEIKH MUHAMMAD AL-JIBAALY

WANAUME: Wanaume ndiwo wanaostahiki kuuteremsha mwili wa maiti ndani ya kaburi, hata akawa maiti huyo ni mwanamke. Kuna sababu nyingi za jambo hili, yakiwemo miongoni mwayo yafuatayo:

a. Huu ulikuwa ndio mwenendo wa Waislamu tangu zama za Mtume (صلى الله عليه وسلم), kama ilivyokuwa mfano wa Abu Twalha (رضي الله عنه) hapo chini (katika sehemu inayozungumzia kuhusu kujamiiana Mke na mume).

b. Wanaume wana nguvu kuliko wanawake kwa kazi hiyo.

c. Lau kama kazi hii ingelikuwa ifanywe na wanawake, baadhi ya sehemu zao za mwili zingelidhihirika kwa wasiokuwa mahram zao katika shughuli hiyo.

d. Haikupendekezwa kwa wanawake kufuata Jeneza, jambo ambalo lenye kukatiza kuwepo kwao wakati wa mazishi.

JAMII: Jamii ya maiti ndio wenye haki zaidi ya kumshukisha maiti wao ndani ya kaburi. Hukmu hii imetokana na maana ya ki-Ujumla ya Aya ifuatayo: **"Na ndugu wa nasaba wanastahikiana wenyewe kwa wenyewe."** [al-Anfaal (8:75) na al-Ahzaab (33:6)].

Kulingana na ma-'Ulamaa wengi, kama vile Ibn Hazm na an-Nawawee, wale wenye uhusiano wa nasaba ni: Baba na baba zake na watoto wa kiume na watoto wao wa kiume, kisha ndugu wa kiume kutokamana na wazazi wote wawili, kisha ndugu wa kiume wanaotokamana na baba mmoja, kisha watoto wao, kisha wajombaze baba na mama wanaotokamana kwa upande wa kuumeni, kisha wajombaze baba wa kuumeni, kisha watoto wao, kisha ni kila mmoja kupita hapo mwenye uhusiano wa ki-damu.

Watatu miongoni mwa jamaa walio karibu na Mtume (صلى الله عليه وسلم) ndiwo waliomshukisha kaburini mwake. Hili lilitajwa kwenye hadeeth ya Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما). Vile vile 'Ali (رضي الله عنه) amenukuliwa akisema: "Mimi nilimuosha Mtume (صلى الله عليه وسلم), na nikatarajia kuona yaliyokuwa ni yenye kuonekana kwa kawaida kwa watu waliokufa, lakini sikuona lolote katika hayo. Alikuwa ni mzuri (katika wajihi na manukato) katika uhai wake na kufa kwake. Kati ya watu wote, waliochukuwa hadhari ya kumshukisha na kumzika ndani ya kaburi lake walikuwa ni wanne: 'Ali, al-'Abbaas, al-Fadhl, na Saalih - mtumishi wake Mtume (صلى الله عليه وسلم). Mtume (صلى الله عليه وسلم) alichimbiwa *lahd* yake, na akaegemezewa matofali nyuma yake." Amepokea 'Abdur-Rahmaan Bin Abzaa yakwamba aliswali nyuma ya 'Umar Ibn al-Khattaab (رضي الله عنه) mjini al-Madinah walipokuwa wakimswalia Zaynab Bint Jahsh (رضي الله عنها). Alileta *Takbeer* Nne. Kisha akamtuma mtu ende akawaulize wakeze Mtume (صلى الله عليه وسلم), "Mwamtaka nani amshukishe kaburini mwake?" Alitarajia yeye mwenyewe bi-nafsi kufanya hilo, lakini wakamjibu, "Angalia aliyekuwa akiruhusiwa kumuona alipokuwa katika uhai wake, ndio umruhusu amshukishe kaburini mwake." Akajibu ('Umar), "Mumepata jawabu la sawa!"

MUME: Inaruhusiwa kwa mume amshukishe mkewe aliyekufa ndani ya kaburi lake. Amesimulia 'Aaisha (رضي الله عنها) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimjilia katika siku maradhi yake ya mwisho yalipoanza. Alilalamika kuhusu alivyokuwa akiumwa na kichwa kwa kusema, "Aah Kichwa changu!" Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamjibu: *"Natamani kama hilo (suala la mauti) lingelikujilia wewe wakati mimi ningelikuwa hai. Hapo basi, mimi ningelikutayarisha na kukuzika."*

Suala hili lilishtua wivu wa 'Aaisha(رضي الله عنها) mpaka akasema, "Nilikutarajia katika siku kama hii ukajifurahisha na mmojawapo wa wake zako." Kisha akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"(Kwa hakika) ni kichwa changu chenye kuuma! Hebu niitie mimi babako na ndugu yako ili nipate kuandika barua (ya uteuzi) kwa Abu Bakr, kwa sababu mimi nahofia asije akasema msemaji na akatamani mwenye kutamani (yakwamba), "Mimi nastahiki zaidi (katika uongozi)!" Lakini Allaah (عزّ وجلّ), na vilevile waumini, watamkataa mtu yoyote asiyekuwa Abu Bakr."*

HAKUNA KUINGILIANA (KI-MAPENZI): Ni katika sharuti kwa mtu (mwanamume) mwenye kuingia kaburini kuuzika mwili asiwe alifanya kitendo cha kujamiiana kimapenzi na mkewe muda mchache karibuni. Ikiwa jamaa wa karibu watashindwa kutekeleza sharuti hilo, wengineo watakuwa na haki zaidi ya kuuzika mwili, hata kama (aliyekufa) alikuwa ni mwanamke na hawakuwa mahram zake.

Amepokea Anas (رضي الله عنه) yakwamba alishuhudia mazishi ya mmojawapo wa mabinti wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) {nae alikuwa ni Umm Kulthum, mkewe 'Uthmaan, aliyekufa katika mwaka wa 9 H}. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikaa pambizoni mwa kaburi, akibubujikwa na machozi, kisha akauliza, *"Kuna mtu miongoni mwenu ambaye hakumkurubia mkewe katika usiku wa jana?"* Akajibu Abu Twalha,

YALIYOMO

MAZISHI	1 - 2
KUPOTEZA WAKATI	2
MKASA NI MTIHANI?	2
NDOA BILA YA WALEE	3
KHUTBAH YA IJUMAA	4

"Mimi sikufanya, Yaa Rasoolullaah!" Akamwambia, *"Haya basi ingia ndani ya kaburi lake."* Nae akaingia kaburini na kumzika.

Katika riwaya nyengine ya tukio hili, Anas amesema yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Mtu yoyote aliyemkurubia mkewe katika usiku wa jana, hafai kuingia ndani ya kaburi."*

Kwahiyo, 'Uthmaan (رضي الله عنه) hakuingia kaburini (kumzika mkewe).

{**TANABAHI** yakwamba baadhi ya riwaya zimesimulia yakwamba jina la binti huyu ni Ruqayyah, ambayo ni makosa kutoka kwa mmojawapo wa wapokezi, kwa sababu Ruqayyah alikufa wakati Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipokuwa kwenye vita vya Badr, kwahiyo hakuhudhuria katika mazishi yake}. Imaam an-Nawawee akaeleza: "Hii ni mojawapo ya hadeeth zilizotumiwa kama dalili yakwamba wanaume ndiwo wenye kutekeleza mazishi, hata kama aliyekufa alikuwa ni mwanamke. Ni maarufu yakwamba Abu Twalha (رضي الله عنه) hakuwa ni mahram ya bintiye Mtume (صلى الله عليه وسلم), lakini alikuwa ni mmojawapo wa watu wema waliokuwepo. Hapakuwa na mahram isipokuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم), ambaye huwenda ikawa alikuwa na sababu ya kutoingia ndani ya kaburi lake - na vilevile mumewe 'Uthmaan. Inajulikana mno yakwamba dada yake, Faatimah, na wanawake wengine walikuwa wanapatikana, jambo lenye kuashiriya yakwamba wanawake hawafai kuingia kaburini na kuzika."

Al-Haafidh Ibn Hajar akasema: "Hadeeth hii inaashiriya yakwamba mtu ambae hivi karibuni hakuwahi kutekeleza tendo la kujamiiana (kimapenzi) na mkewe, hufadhilishwa kuliko baba na mume (wa aliyekufa) katika kutekeleza mazishi, hata kwa mwanamke."

HUKMU YA KUPOTEZA WAKATI NA MICHEZO KWENYE SIMU ZA RUNUNU NA MICHEZO YA COMPUTER 'PLAYSTATION'

Na: Sheikh Mashhoor Hasan Aal-Salmaan

[Endelea kutoka Volume 22, Issue 2]

Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia: *"Hutofikwa na kupoteza mara mbili kuzidiwa nguvu na kuchukuliwa mali yako."*

Rukaanah alikuwa ni mtu ambaye hakuwahi kushindwa na yoyote, na hapakupatikana aliyeweza kumbwaga chini kwenye ardhi. Ndugu zangu wamenisimulia kuhusu M-misri mmoja waliyemuona kwenye 'Internet', alikuwa akiishi kwenye milima ya Misri, alikuwa na ngumi yenye uzito kuliko nyundo! Na kwamba lau ataupiga ukuta ngumi basi alikuwa akiubonyeza! Na waliniambia yakwamba alkuwa akiweka sarafu (ya fedha au shaba) baina ya kigubiko chake cha jicho (*jafan*) na shavu lake la uso (*Khad*) na akaikunja na kisha kuibananga kwa mikono yake!

Baadhi ya watu wana nguvu za ajabu kama mtu mwenye wake wanne na akawa na uwezo wa kustarehe nao wote kwa zaidi ya mara kumi na tano! Huyu ana uwezo wa kupita kiasi!

Vilevile ndivyo alivyokuwa Rukaanah, kwani Mtume (صلى الله عليه وسلم) limbwaga chini kwa mara ya kwanza, nae hakuamini, kisha likafanyika tena hilo kwa mara ya pili na kisha katika mara ya tatu Rukaanah akasema: "Mimi nashuhudia yakwamba wewe ni Mtume wa Allaah!".

Kwahiyo, kupigana miereka ni jambo lililofanywa na Mtume (صلى الله عليه وسلم), linakuwa halina ubaya, bali mimi nawahimiza ndugu zangu miongoni mwa vijana wawe ni wenye kutekeleza mila ya Muhammad kama vile kupeleka Farasi, kukimbia, kupigana miereka bila ya kusababisha madhara. Haya ni bora kuliko kucheza mpira na michezo mengine. Daima-dawama sisi husema *Uongofu bora ni uongofu wa* Mtume (صلى الله عليه وسلم)" - kwahiyo huu ni uonofu wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuhusiana na michezo! Michezo hii ni bora hata kuliko michezo ya aina nyengine bila ya shaka! Ina faida nyingi kuliko michezo mengine na huleta uchangamfu kuliko mchezo mwengine wowote kwa sababu hili ndilo ambalo Allaah alilompa Mtume wake (صلى الله عليه وسلم).

Ama kuhusu michezo mengine kama vile kandanda, basi mimi nimesema yakwamba kunapatikana ndani yake mambo yaliyoharamishwa na vitendo vitatu vilivyoharamu ndani yake ni yafuatayo:

1. Kupoteza wakati na nguvu, ongezea na idadi ya watazamaji na uongezee muda wote wa mchezo wenyewe = muda wa wakati uliopotea - hususan paiwemo na marudio ya michezo hiyo!
2. Ukosefu wa uadilifu katika mizani, kwani mchezaji kandanda hufanywa kuwa ndiye shujaa mkubwa!
3. Husababisha ushabiki wa uanachama na ujinga baina ya watu na mara nyengine hata baina ya nyumba moja! Twamuomba Allaah atusalimu salama! Uadui baina ya mtu na Nduguye na hata mara nyengine baina ya Mtu na Mkewe!? Twamuomba Allaah Atulinde na hayo.

NI LINI MJA ANAPOTAMBUA YAKWAMBA MKASA NI MITIHANI AU NI ADHABU?

Na: Sheikh Abdul'Azeez bin 'Abdullaah Bin Baaz (رحمه الله)

SUALI: Mtu akitiwa kwenye mitihani ya maradhi au akidhurika na jambo baya katika mwili wake au mali yake, atajuaje ikiwa mtihani huu ni majaribio au hasira zitokazo kwa Allaah?

JAWABU: Allaah (عزّ وجلّ) huwajaribu waja wake wakiwa katika ne'ma na na dhiki, katika mambo mazito na usahali. Mara nyengine huwajaribu kwa mambo haya ili apate kuwainua daraja zao na kupandisha hali za watu hao na kuzifadhilisha mara dufu 'amali zao. Kama alivyofanya Allaah kwa Manabii na Mitume wake (عليه الصلاة والسلام), na vilevile watu wema miongoni mwa wenye kumuabudu Allaah.

Kama alivyosema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Wenye kupata mitihani mizito zaidi katika watu ya kusukwa kusukwa ni Mitume, kisha ni wale wenye kuwafuata wao kwa daraja, kisha ni wenye kufuata."*

Wakati mwengine Allaah hufanya hivyo kutokana na madhambi na dhulma za watu, ili adhabu ipate kuharakishwa. Kama alivyosena Allaah: **Na kila mufikwapo na balaa, ni kwa sababu ya yaliyoyatuma mikono yenu. Nae husamehe mengi."**

Kwahiyo,ilivyo kwa ujumla kwa mwana-adamu ni kwamba wao ni wapungufu, na wao hawatekelezi majukumu yote. Kwa hivyo, yenye kuwadhuru wao ni yenye kutokana na madhambi yao na makosa kulingana na amri za Allaah. Na ni kwa ajili hii, ndipo, ikiwa mtu miongoni mwa waja wema wa Allaah atakumbwa na maradhi au kitu chengine

mfano wake, basi hii inatokamana na sampuli ya mitihani iliyowapata Mitume na Manabii, kuinuka kwa daraja zao na kuzidishiwa katika malipo yao, zipate kuwa ni mifano kwa wengine katika kuwa na subira na kukinai.
Kwahiyo, kwa ufupi, huwenda ikawa ni mtihani ili daraja zipate kuinuliwa na kuyafanya malipo kuwa ni makubwa, kama ambavyo Allaah anavyowafanyia watu wema. Huwenda ikawa ndiyo kafara ya madhambi yao, kama ilivyotajwa katika maneno yake Allaah (سبحانه وتعالى): **"Mwenye kufanya maovu, atalipwa kama alivyofanya."**
Vilevile katika hadeeth ya Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Muislamu hapati msiba wa dhiki, wala huzuni, wala maradhi na wala mazito, wala majonzi wala madhara yoyote isipokuwa Allaah humfutia kwa madhambi yake hata kwa mwiba unaomdunga."*
Hadeeth ya Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Yoyote ambaye Allaah Amtakiae mazuri, basi humuingiza kwenye mitihani."*
Huwenda ikawa hii ni adhabu iliyoharakishwa kutokana na udhalimu uliotekelezwa na mja na asifanye haraka kutubia kama ilivyotajwa katika hadeeth ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) - yakwamba alisema: *"Allaah amtakiapo mja Wake mambo mazuri, basi huiharakisha adhabu yake katika ulimwengu huu, na Allaah akimuandikia mja wake maovu, basi Allaah huzuiya madhambi yake mpaka amfidie katika siku ya Kiyama."*
Imepokewa na at-Tirmidhee na akaithibitisha kuwa ni *hasan*.
Kila sifa njema inamstahiki Allaah, Swala zake na Salamu zimfikie Mtume wetu wa mwisho Muhammad (صلى الله عليه وسلم), Ahli zake, Maswahaba zake, na wote wenye bkuufuata uongofu wake.

KUOA PASI NA IDHINI YA WALEE WALA MASHAHIDI

Na: Sheikh Mash-hoor Hasan Aal Salmaan

Ndugu yetu mmoja kutoka katika mji wa *Ramallaah* nchini Palestina, na twamuomba Allaah Aurudishie Uislamu na Waislamu, auliza:
SUALI: Mimi ni ndugu yenu wa ki-Palestina, "Multazim" (mwenye kujifungamanisha na misimamo ya dini) na umri wangu ni miaka 28 na kila sifa njema ni yenye kumthubutukia Allaah kwa baraka kama hizi. Mimi nimependana na mwanamke aliyewachwa na ana watoto, na sijaowa bado. Lakini hatahivyo, kuna mambo fulani yenye uzito yanayotuzuiya sisi tusiowe waziwazi, hata kama kuna mashahidi pia. Mambo hayo yamefikia kiwango ambapo hata twaweza kuuwawa hatahivyo, sisi twapendana na twataka kuoana hata kama atakaejua ni Allaah Peke yake yakwamba tumeowaqna. Kwahiyo kwa kiwango cha ilimu ambacho, hapana mzaha ndani yake, mwanamke huyu alicho nacho kunizidi mimi, tumeamua kukuuliza wewe: Jee, ndoa yetu mbele ya Allaah itakuwa halali ikiwa atasema mbele yangu: "Mimi najioza kwako juu ya Sunnah ya Allaah na Mtume wake kwa kiwango kadhaa cha Mahari" na na yakubali haya, na Allaah ni Mbora wa mashahidi, nikisema, "Juu ya Sunnah ya Allaah na Mtume wake, mimi nakubali kukuowa wewe kwa Mahari tulokubaliana nayo? Hii ni kwa sababu sisi hatutaki mtu yoyote ajue kuhusu ndoa yetu isipokuwa Allaah na twataka uhusiano wetu uwe ni halaal, na twazungumza na kuonana, ama kuhusu sisi kuitangaza ndoa yetu ni jambo lisowezekana kwetu sisi kulifanya kwani litasababisha mauti juu yetu, hata kama twalifanya kulingana na wahyi kutoka kwa Allaah. Sisi twatarajia yakwamba utatusaidia katika suala hili, Ewe Sheikh muheshimiwa, na twamuomba Allaah akuongoze katika kulifanya lile lililo zuri na kuitumikia dini ya Allaah (سبحانه وتعالى).

JAWABU KUTOKA KWA SHEIKH MASH-HOOR:

Kwanza kabisa, hilo neno "Multazim" halijasikika kwenye vitabu, na pili watu wengi hutumia neno "Multazim", haliyakuwa ni Tazkiyah, kwahiyo ni kama kwamba mtu anajichukulia yeye kuwa ametakasika.
Akhee, *Baarakallaahu Fiykum*, uhusiano wako hivi sasa ni wa ukaidi na inakupasa uzingatie kuhusu kudhihirika huko mbeleni kuwa kwenye Sunnah ya Shaytan, ambapo Allaah hana fungu lolote hapo! Utakapokutana nae (huyo mwanamke) na kuzungumza nae: "Mimi nitakuowa kwa Sunnah ya Allaah na Mtume wake (صلى الله عليه وسلم), na pia ukawa ni Mzinifu iwapo utasema, "Nimekubali kukuowa juu ya msingi wa *mahr* haya pasi na kuwepo walee (msimamizi / mlinzi) katika hali hiyo, bila ya mashahidi wowote na bila ya kuitangaza ndoa yenyewe - kwani hali zote hizi ni miongoni mwa masharuti ya usawa wa ndoa (katika Sheriya ya kidini).
Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Hakuna nikaah bila ya kupatikana ruhusa ya walee na mashahidi wawili."*
Kwahivyo, ni sharuti apatikane walee, na si lazima walee huyo awe ni baba, kwa sababu ikiwa baba amekufa au atashindwa kumuoza binti yake, basi mjombake, ndugu yake au kiongozi wa ki-dini ataweza kumchukulia majukumu kwa niyaba yake na ambae awezae kutafutwa kwa niyaba yake kuhusiana na kumuoza, hili linatosheleza. Ndoa si *Mut'ah* baina ya mume na mke, bali ndoa ni *Musaaharah* (kuwakataza wanaume kuwaowa wanawake fulani) na hujenga mafungamano baina ya jamii mbili na ndoa vilevile ina matunda na baraka, kama vile watoto. Ama kwa upande wake jinsi alivyojitokeza mbele yako, basi hili ni jambo ambalo halikuruhusiwa na ni makhsusi kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم).
Kwa bahati mbaya imekuwa ni jambo lililoenea katika kila pembe ya ulimwengu, hususan kwenye miji ya ki-Magharibi, kuwaona Waislamu *wakihalana* na "vipusa" vyao na kujaribu kuwalazimisha jamii nzima iwakubalie hayo, hata kama hakuna nafasi ya jamii hizo kuyakubali hayo. Hawa wenye kuleta utata huu huzidi kutia uchungu pale wanapowahusisha wale walinganizi wa Da'wah *"ma-du'aat"* wanaodai ati kulingania kwenye *Sunnah*, *Salafiyyah* na *Jihaad*, kwa ghafula wanaposahau aibu zote na kutafuta kusawazisha matamaniwa yao ya kupotelea mbali kwa kuifagia misingi ya ki-Sheriya chini ya mazulia.

"...na (tumekuhalalishia kila) mwanamke Muislamu akijitoa mwenyewe bure kwa Mtume, kama mwenyewe Mtume akitaka kumuowa. Ni halali kwako tu (kumuowa mwanamke bure bila ya mahari) si kwa Waislamu wengine."
[Al-Ahzaab 33:50]

Katika Musnad Ahmad, kutoka kwa Anas, alikuja mwanamke mmoja akitaka kujitolea kuolewa na Mtume (صلى الله عليه وسلم), mara binti yake Anas akasema: "Ni mwanamke gani yule aliyekosa haya!?" Akasema Anas, "*Wallahi* mwanamke yule ni bora kuliko wewe!" Kwa maana yakwamba: Wataka kuwa mke wa

Mtume (صلى الله عليه وسلم) hiyo si aibu. Kwahivyo kwa mwanamke kujitolea kutaka kuolewa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) limeruhusiwa ingawaje hivi ndivyo alivyosema Allaah:

Ni halali kwako tu (kumuowa mwanamke bure bila ya mahari) si kwa Waislamu wengine."

[Al-Ahzaab 33:50]

Hili ni kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) peke yake, ama kuhusu Waislamu wengine waliobaki, basi hapana budi apatikane walee na mwanamke yoyote atakaejiozesha mwenyewe bila ya ruhusa ya walee wake atakuwa ni mzinifu. *Na lau kama yule mume (ataingiliana nae kimapenzi), basi mahari yatakuwa ni haki yake kwa sababu ameingia kwenye sehemu zake za siri.* Na hili limetupelekea kwenye mas'ala muhimu sana ambayo ni ikhtilafu ya maoni inayostahiki kuzingatiwa. Umeona jinsi Mtume (صلى الله عليه وسلم) alivyomzungumza mwanamke aliyeolewa kwa njia kama hii kuwa ni Mzinifu, na kisha akasema yakwamba: *"Na lau kama yule mume (ataingiliana nae kimapenzi), basi mahari yatakuwa ni haki yake kwa sababu ameingia kwenye sehemu zake za siri."* Kwanini? Kwa sababu amefasiri mfano wa yapatikanayo kwenye *madh-hab* ya Abu Haneefah, ambapo mwanamke anaweza kuolewa bila ya walee, ingawaje hata kwenye hali kama hii kuna mashahidi na kutangazwa kwa ndoa pia kukapatikana. Ama kukosekanapo mashahidi au ndoa yenyewe isitangazwe na mwanamke huyu akikwambia, "Mimi najitolea kuolewa na wewe".

Huu ni uzinifu ambapo mwanamke hupewa zawadi yake kadiri ya alivyoshiriki. Kwahiyo ndugu yangu, "Baarakallaahu Fiyk" mche Allaah na wala usiungie mlango huo, jitayarishe na upange na wazazi wako, walee wake na uingie kwenye nyumba kwa kupitia katika mlango wake wa kisawasawa na wala usiingie kwenye mlango mwengine ambao usokuwa ni wa kisawasawa kuingiliwa.

"Tenganisha! Tenganisha!"

[Ndoto ya Sheikh Al-Albaani]

Siku moja Sheikh Al-Albaani alisema, "Nilikuwa nikiumwa na jicho, kwahiyo daktari akaniamuru nichukuwe mapumziko kwa muda, yaani nisiandike wala nisisome. Nikajiambia [nafsi yangu]: ili wakati usinipite kwa kuupoteza, nitampa mmojawapo wa ndugu zetu waraka mdogo ili anakili maandiko yake, kiasi cha kwamba atakapomaliza, nitakuwa nimepumzika vya kutosha.

Yule ndugu akaanza kuandika kwa kuiga ule waraka, na mimi nikawa nafuatiza kwa kuangalia alichonukuu, na huku nikijifariji nafsi yangu kwa kusema yakwamba kusoma huku hakutoniathiri [vibaya] jicho langu au kuniharibu nguvu za macho yangu. [Wakati nilipokuwa nikifanya hayo] Nikaliona neno moja [kwenye ule waraka unaoandikwa] ambalo sikulifahamu na pia sikuweza kulisoma [neno hilo]. Nikarudi kwenye ule waraka asilil na nikaona yakwamba yule ndugu amenukuu lile neno [sawasawa] kama lilivyokuja kwenye waraka, kwa hakika alikuwa ni muandishi mzuri.

Nikaanza kuliangalia lile neno na kuvuta fikra zangu na kulizingatia, nikitumai yakwamba nitavumbua njia ya sawa ya jinsi ya kulisoma neno hilo. Lakini nikashindwa nikawa nimeshughulishwa nalo mno.

Usiku ulipoingia, nikenda zangu kulala, mara nikaamka kutoka usingizini na huku nikawa nasema, "Tenganisha, tenganisha! Tenganisha, tenganisha!" Sikuifahamu vyema ndoto hiyo? Basi nikasema [kujiambia nafsi yangu], 'Ewe Naasir, hebu andika yaliyotokea,' ili nisije nikaisahau ndoto yangu, na kukipambazuka nitajaribu kuiangalia ilikuwa na maana gani.

Kwa kweli kulipopambazuka nikaanza kufikiria na nikasema: Labda huwenda ile ndoto ikawa na mafungamano na lile neno gumu [nilojaribu kulisoma kwenye ule waraka]. Nikauleta ule waraka na nikaanza kuliangalia lile neno gumu [mara papo hapo], nikaanza kulirudia-rudia lile neno [nililokuwa nikilisema pindi nilipoamka kutoka usingizini, yaani, 'Tenganisha!'] mpaka nikafikia kwenye suluhisho la tatizo. Neno lilo-onekana kwenye ule waraka [kwa hakika] lilikuwa ni maneno mawili yaliyo unganishwa na muandishi, kwahiyo nikayatenganisha na nikaweza kulisoma na kulifahamu.

KUZUNGUMZA BAINA YA KHUTBA MBILI SIKU YA IJUMAA?

Na: Sheikh Mashhoor Hasan Aal-Salmaan

SUALI: Tuseme nini baina ya Khutba mbili za Ijumaa? Tuombe msamaha (istighfaar) kutoka kwa Allaah au tusome Surat al-Faatihah? Na Jee, twaruhusiwa kuzungumza baina ya Khutab mbili?

JAWABU: Na'am, ndio inaruhusiwa kuzungumza baina ya Khutbah mbili. Hukmu inayohusiana na Khutbah ni kwamba twatakiwa kuwa kimya, lakini ama kuhusu baina ya khutbah mbili, hapana kilichotajwa kwenye Sheriya - kwahiyo, fanya upendavyo.Ukipenda kuzungumza, hiyo ni juu yako na ukipenda kumkumbuka Allaah, hiyo pia ni juu yako. Na sisi hatufanyi kitu chochote (makhsusi) kwa njia ya Ibaada (katika wakati huu). Ama kuhusu hadeeth isemayo, *"Pindi Imaam anapopanda juu ya Minbar, hapana swala wala mazungumzo."*

Basi hadeeth hiyo ni ya urongo. [Silsilah adh-Dhaifa : 87]

Na katika zama za 'Umar ibn al-Khattaab (رضي الله عنه): Watu walikuwa wakizungumza baina ya khutbah mbili - nae ('Umar) alikuwa juu ya Minbar. Ingawaje, hatari na madhara ni kuzungumza haliyakuwa huku Imaam anatoa khutbah yake.

Ama katika Swaheeh; kutoka katika hadeeth ya Abu Hurairah (رضي الله عنه) isemayo: *"Ukimwambia ndugu yako, haliyakuwa Imaam anatoa khutbah "Nyamaza", basi wewe mwenyewe utakuwa umefanya laghw (kitendo kiovu)* [Swaheeh al-Bukhaaree [2: 56]].

Kwahiyo, mazungumzo hayafai wakati Imaam anapotoa khutbah. Lakini anapokaa baina ya khutbah hizo mbili; hapo basi mazungumzo huwa yanafaa.

Na Allaah Ndiye Mjuzi bora wa haya.

Asili: Fataawa 100 za Shaykh Mashhoor Hasan,